



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC**



IMETHIBITISHWA ISO 9001:2015

TAARIFA KWA UMMA

MWALIKO WA KUSHIRIKI KATIKA KIKAO CHA KUKUSANYA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA NAULI ZA ABIRIA NA MIZIGO KWA MELI YA MV. LIEMBA INAYOTOA HUDUMA ZIWA TANGANYIKA

Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) limepokea kutoka Kampuni ya Meli Tanzania (TASHICO) maombi ya viwango vya nauli za abiria na mizigo kwa safari za meli ya **MV. Liemba**. TASHICO imeeleza kuwa mapendekezo yaliyowasilishwa yanalenga kuiwezesha MV Liemba, ambayo ilikuwa imesimama kwa muda mrefu, kutoa huduma endelevu za usafiri wa abiria na mizigo katika Ziwa Tanganyika.

Kwa mujibu wa kifungu cha 29 (2) (b) cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura 415, Shirika limeandaa mikutano ya wadau wa huduma ya usafiri majini katika Ziwa Tanganyika ili kukusanya maoni kuhusu maombi yaliyowasilishwa. Mikutano hiyo itafanyika kama ifuatavyo:

- (i) **Kigoma Mjini** - tarehe 20 Oktoba, 2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa *Kigoma Social Hall* – Kigoma Mjini kuanzia saa 4 kamili asubuhi; na
- (ii) **Nkasi Mjini** - tarehe 23 Oktoba, 2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa Sezero - Kilando, Mkoa wa Rukwa kuanzia saa 4 kamili asubuhi.

Kwa tangazo hili wadau wote mnaalikwa kushiriki. Wadau wanaweza kutuma maoni kwa njia ya mtandao kupitia barua pepe tariff@tasac.go.tz au kwa kufika katika ofisi za TASAC – Kigoma Mjini, Rukwa Mjini au TASAC – Makao Makuu. Maoni pia yanaweza kutumwa kwa njia ya barua kwa anuani ifuatayo: Mkurugenzi Mkuu, TASAC, S.L.P 989, Dar es Salaam.

Mwisho wa kupokea maoni ni tarehe 30 Oktoba, 2026.

Imetolewa na

**MKURUGENZI MKUU
TASAC**